**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**612** **URAIA**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka: 2008**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu **B** na **C.**
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Eleza kwa hoja nne, jinsi utawala bora unavyoimarisha ustawi wa wananchi katika Jamii.

2. Taja vipengele vinne vya haki za kiraia kama vinavyoelezwa katika Katiba ya Tanzania.

3. Onyesha hoja nne zinazoeleza umuhimu wa uwajibikaji kwa viongozi wa umma.

4. Taja mambo manne yanayochukuliwa kama viashiria vya rushwa katika jamii.

5. Kwa hoja nne, fafanua athari za kutofuata taratibu za matumizi ya fedha za umma.

6. (a) Eleza maana ya maamuzi ya pamoja katika jamii.
   (b) Taja njia tatu zinazotumika kufanya maamuzi ya pamoja katika jamii mbalimbali.

7. Onesha kwa hoja nne umuhimu wa elimu ya uraia katika kuimarisha demokrasia shuleni.

8. Taja sifa nne za viongozi wenye maadili mema katika ngazi ya jamii.

9. Onyesha hoja nne zinazoeleza nafasi ya vyombo vya habari katika kukuza uwazi nchini.

10. Bainisha faida nne za kutumia vyanzo mbalimbali vya maarifa katika ufundishaji wa uraia.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** katika sehemu hii

11. Eleza kwa hoja tano umuhimu wa Serikali kuwahusisha wananchi katika kupanga bajeti.

12. Chambua athari tano za mgawanyiko wa kijamii unaosababishwa na itikadi kali.

13. Kwa hoja sita, eleza jinsi shughuli za asasi za kiraia zinavyosaidia kulinda haki za binadamu.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** katika sehemu hii.

14. Bainisha mambo matano ya kuzingatia wakati wa kufundisha somo la uraia kwa kutumia mbinu shirikishi.

15. Chambua hatua sita zinazopaswa kufuatwa katika kutathmini ufanisi wa zana za kufundishia somo la uraia.

16. Eleza kwa hoja sita jinsi mwalimu anavyoweza kuandaa mazingira salama ya kujifunzia somo la uraia.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org